

Kiswahili

ASb
approved

Msitu Wa Nyoka

Brigid Simiyu
Rob Owen




Kijiji cha Sinyaire kimezungukwa na milima na misitu. Nyoka wengi huishi ndani ya misitu hiyo. Nyoka mkubwa zaidi aliitwa Unyalego na wanakijiji. Nyoka huyu aliwameza mbuzi na kondoo wakiwa wazima.




Siku moja, Apiyo, Ajoh na Atieno walipokuwa wakienda msituni kutafuta kuni, nyanya yao aliwaonya, "Jihadharini na Unyalego. Msichukue chochote kutoka msituni ila kuni."




Wasichana hao walifunganya maziwa, ndizi, viazi vitamu na maji. Wakachukuwa kamba za kufungia kuni na panga kali. Wakaondoka kwenda msituni.



Walipokuwa njani, Ajoh, Apiyo na
Atieno waliongea na kucheka. Ghafla,
Apiyo alisema, "Kimya! Tunakaribia
anakoishi Unyalego."




Ajoh hakuzingatia onyo la nyanyake. Atieno aliwaita, "Tazameni, hapa kuna meno ya Unyalego ya dhahabu. Tuyachukue?" Apiyo aliwakumbusha, "Msisahau nyanya ametuonya tusichukue chochote kutoka msituni ila kuni."



Ajoh akajibu, "Simwamini nyanya. Nadhani alisema hivyo ili atuzuie kuchukua tunachotaka. Najua anatuonea wivu. Mimi nitayachukua hayo meno ya dhahabu." Dada zake walikuwa na wasiwasi wakamwonya Ajoh lakini, hakujali.



Baadaye, Unyalego alikuja kutafuta meno yake. Alikasirika alipokosa kuyapata. Unyalego aliwasikia Ajoh, Apiyo na Atieno wakizungumza na kucheka. Akajificha kando ya njia ambayo wasichana wale wangepitia.




Walipokwisha kuzikusnaya kuni,
walizibeba vichwani. Ghafla, wakasikia
"Hzzzzzzzzz!" Walioga wakajaribu
kujificha walimpomwona Unyalego,
kinywa wazi tayari kuwameza.




Unyalego akawauliza, "Ni nani aliye yachukuwa meno yangu ya dhahabu?" Walipokosa kumjibu, Unyalego akaamua kuwadadisi wasichana hao. Akasema, "Ninataka muimbe wimbo. Yule atakaye imba bila kukosea, atakuwa hana hatia na ataenda nyumbani na kuni zake. Atakayekosea, ndiye aliye na hatia na atakuwa chakula changu kwa siku tatu zijazo!"



Apiyo aliimba kwanza kwa sauti nyororo: Sio mimi, sio mimi niliyeiba meno, aliyeiba yuko hapo nyuma aaaah. Kisha Atieno akaimba: Sio mimi, sio mimi niliyeiba meno, aliyeiba yuko hapo nyuma aaaah.



Mwishowe, ilikuwa zamu ya Ajoh. Kwa uwoga alisongea mbele na kuanza kuimba: S.i.o mi-mi, s.i.o. Aliimba vibaya akashindwa kuyatamka maneno sawa. Unyalego akamkemea, "Mbona huimbi vizuri kama wengine?"



Papo hapo, Unyalego akammeza Ajoh. Atieno na Apiyo walikimbia kijijini kueleza yaliyotokea.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Msitu Wa Nyoka

Author - Joseph Sanchez Nadimo

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Rob Owen

Language - Kiswahili

Level - Longer paragraphs

© African Storybook Initiative 2015

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

